

## KAZI YA LIKIZO

### KISWAHILI KIDATO CHA SITA

1. Fasihi simulizi ili iweze kutendeka hutawaliwa na mambo makuu Matano. Kwa mifano Dhahiri fafania mambo hayo.
2. Jadili jinsi waandishi wawili wa ushairi wanayodhihirisha ubora na umuhimu wao kwa kuwasaidia wanajamii wa kitanzania katika mbalimbali.
3. “Lengo la hadhira katika kazi ya fasihi ni kuipa uhai kazi husika”. Fafania dhima tatu za hadhira katika upande wa hadithi na dhima mbili za hadhira katika utanzu wa vitendawili.
4. Dhamira ya mapenzi ni moja ya dhamira inayowafikirisha waandishi. Kwa kutumia hoja nne kutok katika kila diwani kati ya diwani mbili ulizosoma thibitisha kauli hiyo.
5. Eleza maana ya ngano. Kisha fafania faida nne (4) za maneno ya kifomula kama sifa mojawapo ya ngano.
6. Jadili dhana ya fadhila kama ilivyojitokeza katika vitabu viwili vya ushairi ulivyovisoma. Tumia hoja nne kwa kila kitabu.
7. “Watetezi wa nyakati zako wanasulubiwa kabla ya kuonesha suluhisho alilokusudia mwandishi”. Fafania hoja hiyo ukihusisha tamthiliya mbili (Hoja nne kwa kila hoja)
8. Tamthiliya ulizosoma zimepitwa sana na wakati. Jadili ukweli wa kauli hii kwa kutumia tamthiliya mbili ulizosoma (Toa hoja nne kwa kila hoja)
9. Jamii isiyo na maadili ni jamii mfu. Jadili namna washairi wa diwani mbili ulizosoma walivyoshughulikia suala la maadili. (Toa hoja nne kwa kila kitabu)
10. Ushairi ni msingi wa maneno ya hekima kwa jamii yako. Thibitisha usemi huo kwa kutoa hoja nne kwa kila diwani kwa diwani mbili ulizosoma.
11. Tumia hoja tano kuonesha tofauti kati ya hadhira ya fasihi simulizi na hadhira ya fasihi andishi.